

## **MAKTABA KUU -- ZANZIBAR**

### **KANUNI ZA KUJIUNGA NA UANACHAMA WA MAK TABA**

- 1) Kila anaetaka kujiunga na uanachama wa maktaba atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo inapatikana katika dawati la mapokezi.
- 2) Fomu hiyo utatakiwa uirejeshe pamoja ikiwa na picha moja ya (passport size) itakayo tumika katika kutengenezea kitambulisho (IDENTITY CARD) ambacho utatakiwa kuwa nacho unapokuja kupata huduma za maktaba.
- 3) Fomu hiyo lazima iwe na muhuri halali wa skuli, ofisi au muhuri wa sheha katika eneo unalotoka.
- 4) Utatakiwa kuandika namba yako ya simu ya halali na ya mdhamini wako. Namba hii ituwezesha kukupata pindi kukiwa na haja ya kufanya mawasiliano na wewe.

### **GHARAMA ZA UANACHAMA**

- 5) Wanafunzi wa Vyuo na wengineo ada yao ni **TSH 15,000/=**
- 6) Wanafunzi wa Secondary FI -FVI **5,000/=**
- 7) KG – STD VI TSH **1000/=**

### **GHARAMA ZA USAJILI WA TAASISI**

- 1) Kifurushi cha **Platinum** TSH **300,000/=**
- 2) Kifurushi cha **Gold** TSH **200,000/=**
- 3) Kifurushi cha **silver** TSH **100,000/=**

### **KWA WAGENI**

- 8) Kwa upande wa wageni watalipia TSH **30,000/=**
- 9) Uanachama utakaopewa utadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu na utalazimika kuongeza muda wa uanachama uliopewa kwa kulipia nusu gharama ulizolipa wakati wa kuomba uanachama.
- 10 ) Kila mwanachama atapatiwa kadi mbili (READERS TICKETS) zitakazomuwezesha kuazima vitabu viwili kwa wakati mmoja

### **KANUNI ZA UTUMIAJI WA MAK TABA**

- 1) Hifadhi mikoba yako katika dawati la mapokezi,ni marufuku kabisa kuingia ndani ya maktaba na mikoba ,mifuko au vifurushi.

2) Ni wanachama tu ndio watakaoruhusiwa kuazima vitabu na idadi ya mwisho ya vitabu vyatua ni viwili(2) kwa wakati mmoja.

3) Taasisi itakayojiunga na kifurudhi cha **Platinum** atapata huduma ya kuazimwa vitabu **50** kwa **mwezi**, mafunzo na kupangiwa maktaba yake. Kifurushi cha **Gold** atapata kuazimwa vitabu **30** kwa **mwezi**, kupangiwa maktaba na ushauri wa kitaalamu. Kifurushi cha **silver** atapata huduma ya kuazima vitabu **20** kwa **mwezi**

4) Muda wa kuazima vitabu ni wiki mbili na baadhi ya vitabu ni wiki moja na lazima virudishwe si zaidi ya tarehe iliyonyeshwa nyuma ya kitabu.

5) Iwapo mwanachama atahitaji kuongeza muda wa kukaa na kitabu/vitabu ni lazima avirejeshe maktaba kwa kuongeza muda.

6) Atakaechewesha kurejesha kitabu/vitabu atalazimika kulipa faini ya Tsh. **1000** /= kwa siku kwa kila kitabu na hataruhusiwa kuchukua kitabu kingine akishindwa kulipa faini hiyo uanachama wake utasimamishwa hadi hapo atakapolipa faini hiyo.

7) Ikiwa mwanachama hatotumia uanchama wake kwa mwaka mzima na zaidi, atalazimika kulipia gharama za uanachama mpya kwa mujibu wa kiwango chake cha elimu.

8) Ni marufuku kuazima kitabu kwa kutumia kadi ya mtu mwengine.

9) Yeyote atakaebainika kuchukua kitabu kwa nia ya kuiba atachukuliwa hatua za kisheria.

10) Mwanachama atakaepoteza, atakaerudisha kitabu hali ya kuwa kimechanika au kupungua karatasi, atalazimika kukilipa kitabu hicho.

11) Sio ruhusa kuzungumza na simu unapokua Maktaba

12) Hairuhusiwi kula ,kunywa,wala kuvuta sigara ndani ya Maktaba.

13) Ni marufuku kufanya majadiliano kwa sauti kubwa ndani ya Maktaba.

### ZINGATIA :

- Unalazimika kufuata kanuni hizi wakati wote unapokua Maktaba
- Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakae vunja sheria hizi.

Kurejeshwa kwa fomu hii inathibitisha kuwa umezisoma na kuzifahamu kanuni za utumiaji wa maktaba yetu na upo tayari kuzifuata

Tunaomba ushirikiano wako.